**Hon. Mwayaa:** Asante mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ambayo nimeingoja kwa mda mrefu sana. Mheshimiwa Spika, furaha imekaribia moyo wangu wakati Mwenyekiti wa bajeti aliposimama na kusema kitita fulani kimeongezwa katika Idara ya Afya. Kule mashinani, imekuwa ni hali ngumu sana upande wa zahanati zetu; madawa hakuna na hivyo ukienda hospitalini, unakuta madaktari wako ama hata wauguzi wako lakini wanawaandikia makaratsini wagonjwa kwamba wakaangalie madawa mahali kwengine.

Hivyo mheshimiwa Spika, bajeti hii naiunga mkono kwamba inapopita na ninajua itapita, ikasaidie madawa yaweze kununuliwa yapelekwe katika zahanati zetu kwa sababu watu wa Kilifi wamekuwa wakipata shida kubwa sana na hakuna madawa. Unaweza kumwona *lab technician* yuko pale lakini ni kama ambaye yuko likizo maana vile vifaa ya kufanyia kazi haviko na yote tukiuliza tukaambiwa pesa zilikuwa hazitoshi kwa sababu wenye kusambaza madawa wanadai. Mheshimiwa Spika, bajeti hii ikipita haya yote yatapungua na yataenda vizuri kwa sababu tutakuwa tunapata madawa katika zahanati zetu na *labs* pia zitafanya kazi kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, zile *collapsed projects*, kama sisi ambao tumerudi na ni wa zamani hapa, ilikuwa ni aibu wale waliokuwa hawajui kwa nini miradi imekwama walikuwa wanaweza kusema kuwa waheshimiwa wamekula pesa ndio maana miradi haiendi. Tulikuwa tuna miradi

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

mingi ya shule za chekechea, zahanati na miradi ya maji ambayo ilikuwa kule mashinani wodini kwetu. Ilikuwa ukitembea ni aibu watu wanasema labda pesa zilifanyiwa kampeni lakini saa hii imedhihirika wazi kwamba pesa hizi zilikuwa zimetumiwa kulipa madeni ambayo yalikuwa yamelimbikizwa kwa sababu tulikuwa na ukusanyaji duni wa ushuru wetu. Kwa hivyo, hivi saa hii tutakuwa na sura kule mashinani kwamba miradi ile ambayo ilikuwa imekwama mahali itanza hivi karibuni ili kwamba Kilifi yetu iende mbele.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hata wenzetu wanaoishi na ulemavu hawajaachwa nyuma na bajeti hii ambayo tunaipitisha leo. Kumewekwa kitita fulani cha kununua vifaa vyao ili waweze kufikia huduma mbali mbali. Pia sitasahau kwamba maji pia yamewekwa kitita chake. Wakati ule wa kwanza kitita cha maji hapo zamani ilisemekana kimepelekwa kule ambako kuna chemichemi za maji. Lakini saa hii nikisimama hapa, mimi kwangu hakuna chemichemi za maji; nina imani kwamba kitita hiki kitaanza kufanya kazi baada ya bajeti hii kupita kitafikia watu wa Kayafungo na kwengine kwa sababu tayari kwengine kumewekwa mabomba bado sisi kuchukua pale ambapo maji yako na kusambazia maji watu wetu.

Mheshimiwa Spika, tukipitisha bajeti hii leo, tunaimani kubwa wakaazi wa Kilifi watapata huduma ambazo wamezingoja kwa hamu sana, hasa kipindi hiki ambacho ni kama wanaona hatujafanya kazi na ilikuwa ni mpaka bajeti ipite ndio sasa tuanze kazi rasmi. Asante na naiunga mkono, na asante pia Mwenyekiti kwa kuleta Ripoti hii mapema ambapo zamani ilikuwa haifanyiki hivi; pongezi. Asante mheshimiwa Spika.

**Hon. (Ms.) Messo:** Thank you Mr. Speaker. I stand to support the Motion. First of all, I congratulate the wise Chair of the Budget Committee. In this Assembly, we have wise Members that is why we did not have problems about the Budget. This is my first term in the Assembly and I thought that there will be tug of war come budget time; to my surprise everything is calm and cool. There was no lobbying and everything was transparent. Our Chairperson for the Budget Committee has explained to us each and every detail of how we are going to spend our monies in Kilifi.

I am so happy about the PWD (persons living with disabilities) in some other counties I am sure they did not even remember the PWDs and I also thank them for adding more funds to the side of Health. Since we have a very able CEC of Health, I am sure everything will be okay. Now, I beg our Speaker, come next time 2019/2020, for the PWDs they should add more monies since Kshs 3 million is just too little because the way the Chairperson has told us, the number is too big for the Kshs 3 million but I am so happy; better something little than nothing.

So I stand to support and I urge fellow Members let us not waste time. Let's brush it off and we pass it today. We are waiting for this to happen and it is history the Kilifi people will see. Thank you so much my able Speaker.

**Hon. Mwamtsi:** Thank you Mr. Speaker, for giving me this opportunity. First and foremost, may I join those who started speaking by congratulating the Committee on Budget and Appropriations for this far they have brought us. I support this budget. The passage of the budget is one thing and following it up to make sure projects are implemented is another thing. We have seen in this county, projects that were budgeted for in the year 2014 have not been completed upto now. So, even as we stand here ensuring that we pass this Budget, this House has a responsibility to ensure before the year ends on 30<sup>th</sup> June, 2019, these projects are fully implemented.

For the first time, the people of Kilifi will experience the beginning of the building of the stadium in Kilifi Town. That is one of the positives of this budget. As others were saying earlier,

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

it is important that we have flagship projects because flagship projects in one way or the other have big impact on the people ...

*(Hon. Mwamtsi spoke off record)*

We should not forget the rural areas where the bulk of voters are coming from and I think as shown by the faces of this House that has been addressed. So, I stand here in full support of this budget. Thank you.

**Hon. (Ms.) Elina:** Asante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia Bajeti hii nikipongeza Kamati husika ya Bajeti. Mheshimiwa Kiraga na wenzako pongezi sana kwa kazi mliyofanya. Langu ni kusisitiza haswa kule kwa utendaji kazi kwa *Executive*; kama hawatajitokeza kufanya hizi kazi itakuwa kazi bure. Nataka niwaambie waheshimiwa Kamati ya *Finance* wafuatilie kwa Waziri wa *Finance* kile kinachoendelea ili tuone utendaji kazi unapatikana.

Ninavyowaambia, mambo mengi sana haswa upande wa afya hospitali yetu ya Malindi imerudi nyuma tena kama tulikotoka miaka miwili iliyopita. Usiku wa leo nimepeleka mtu ambaye alikuwa amegongwa na pikipiki kule Magarini; Gongoni hakuna ambulensi. Tulipouliza, ikasemekana ilipelekwa Garashi kwa sababu ya mambo ya maji. Tulipompigia simu yule mhusika katika hospitali kubwa ya Malindi tuweze kupata msaada gari iletwe tusaidie yule kijana ikashindikana mpaka nikambeba na gari langu nikamleta hospitali. Nilipofika pale hospitali, hapaonyeshi kwamba ni hospitali pamerudi pachafu sana.

Kwa hivyo, Kamati husika mko na kazi ngumu sana ya kufanya. Tumetenga pesa nyingi za mambo ya afya. Siku moja nilizungumza pale tulipokuwa na mkutano na Waziri nikamuambia umeingia nyumba ya watu ambao hawafanyi kazi. Wewe pia tutakuweka katika kitengo hicho. Nilizungumza watu wakafikiri ni kama matani lakini saa hii akipata nafasi ya kuenda pale hospitali kubwa ndipo atajua matatizo yanaanza wapi na yanaenda wapi. Napongeza Kamati kwa pesa nyingi walizozipanga kwa hii Idara lakini kama *County Executive* haitatumia hizi pesa kama walivyofanya mwanzo mpaka kukaja pesa na zikasemekana zilipiwe madeni, tutarudi nyuma kule tulikotoka.

Ni wakati wetu safari hii, ambaye hatakuwa anafanya kazi katika Idara yake tusimame kidete tumuondoe ili tulete mtu mwingine; ndio kazi ifanyike kisawasawa. Bila kuwa ngangari tutachezewa na *Executive* maana tunawapatia pesa na majukumu na yale majukumu hawayatekelezi. Tulipokuwa na waziri kule Mombasa alizungumza mazuri sana lakini mpaka sasa hatujaona jambo lolote. Kama alivyokuwa anazungumzia mheshimiwa Mramba mambo ya Rain Drops, Kilifi iko na pesa nyingi lakini zinapotea; hatuoni utendakazi mzuri. Tunaomba waheshimiwa tupitishie hii bajeti lakini tutakapokuwa tumeipitisha, tuwafuate nyuma watu hawa ambao watakuwa wanatumia hizi pesa maana kama hatutawafuatilia nyuma, nawahakikishia kipindi kitaisha na mtasema tena sisi tutakuwa kama kipindi kilichopita kwa sababu wanaotufelisha sisi si Bunge hili bali ni *Executive*.

Nampongeza mheshimiwa Kiraga kwa ile mikutano ya uhusiano baina ya yeye, *Executive*, na waheshimiwa; ametueleweshwa kinachoendelea na amechukua mda mrefu kutuelezea ili tuweze kuelewa bajeti hii. Tumeielewa vile tunavyoizungumzia na niwahakikishia kama serikali ya Kaunti hii haitafanya kazi kipindi hiki, mwaka unaofuata mtaenda kwa *public participation* na mtapigwa. Mtachapwa na wananchi kwa sababu wanasikia uchungu kwamba pesa zinatolewa kwa magazeti na zinasomwa lakini hazionekani. Ni mbio za kobe; hazionekani.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Ningeliomba tujitokeze kidete tutetee watu wetu wa Kilifi. Kila kitengo katika bajeti hii kimetengewa pesa mpaka wanaoishi na ulemavu pia wamepata ambayo hii ni historia lakini kusifika kwa hii bajeti ni *implementation* na kama haitafanyika vizuri, ni kama kazi bure. Acheni tufanye kazi, waheshimiwa wa vyama tofauti tofauti tuweke kando, tushikane tusukume gurudumu la Kaunti ya Kilifi kwa sababu *Executive* sisi ndio wembe wao, twataka kuwanyoa ...

*(Hon. (Ms.) Elina spoke off record)*

Pengine yameletwa na *Executive*. Tukitaka kuwanyoa ni sisi, tukitaka kuwachana ni sisi tukitaka kuwapunguza ni sisi. Kwa hivyo, tuwe waangalifu tupitishie. Asante sana mheshimiwa Spika kwa kunipa hii nafasi.

*(Hon. (Ms.) Mbaru spoke off record)*

Mheshimiwa Spika na hili Bunge, toka juzi hii mitambo inatufanya kama ambaye, unajua kama unaongea unaingia mori halafu ule mori ukikatika ati moto umeenda tunaskia kama ambaye hatu...

*(Hon. (Ms.) Mbaru spoke off record)*

Kama pengine watu wa KP (Kenya Power) wanatutaliza najua Bunge hili limenunua jenereta, kama wakati tunaendelea...

*(Hon. (Ms.) Mbaru spoke off record)*

*Inatiza by the way. Thank you very much.*

**Hon. Mae:** Thank you Mr. Speaker. I first want to congratulate our able Chairperson hon. Kiraga, his Vice and my colleagues in the Budget Committee and also our Clerks led by the Fiscal Analyst Mr. Shabaan Mwanengo. This journey was not easy. It started from the public participation and I remember in Matano Mane we were almost attacked and our beautiful Clerk Riziki had to hide behind me...

*(Laughter)*

I was there; it's not a laughing matter. It almost erupted but thank to our able Chair; he had to stand firm and he promised the people that this time round things will not be as usual. In the Budget Committee he had to promise that we have new schedules and things are going to turn around.

Mr. Speaker, reinstating these ward development projects is a plus for us and especially for those of us who are new. It is a plus because these were projects that had been collapsed and now that we are reinstating these projects it is a huge boost for us politically and to our electorates too.

*(The Speaker (Hon. Kahindi) left the chair)*

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

*(The Deputy Speaker (Hon. Kenga) took the chair)*

Mr. Speaker, what remains here is this House to be given that respect which it deserves from the Executive. Immediately when we pass this Motion Mr. Speaker, we want to see its implementation. They will have to find means where they will get funds, we all know we have resources; the local revenue collection so it is not a matter of bringing another supplementary budget after three or four months then we have to collapse our projects. I want this House to be respected and everything that we are going to pass here to be implemented. Finally, I am in full support of this Motion and I urge my fellow Members to support. Thank you.

*(Applause)*

**Hon. Maitha:** Asante mheshimiwa Spika. Nami nasimama kuunga mkono hoja hii. Mengi yamesemwa na waheshimiwa wenzangu lakini wakati nikipitia hii bajeti kuna vitu ambavyo vilikuwa vikitupa shida kule mashinani kama ile nyumba ya Naibu Gavana. Ule mgao ulikuwa juu lakini nashukuru Mwenyekiti wa bajeti alisikiliza maoni ya wananchi na akaipunguza ile bajeti ambayo ilikuwa imewekwa pale.

Tumegundua kwamba; hasa sisi wageni ambao tumeingia hili Bunge la Pili pia tulikuwa tunapata shida kuhusu ile miradi iliyokuwa imepangwa na wale wenzetu ambao walitolewa na wananchi wakati wa zile kura zilizopita.

*(The Deputy Speaker (Hon. Kenga) left the chair)*

*(The Speaker (Hon. Kahindi) took the chair)*

Tulikuwa tunasemekana tumetoa ile miradi waliyoipanga kwa sababyu hatukuwa tumeipanga sisi lakini Mwenyekiti ambaye alikuwa anajua kazi yake na Kamati kwa jumla wakaona ni bora na wakatupa afueni sisi kuregesha ile miradi.

Kwa hili na lile la Naibu Gavana, sitaki kuongea yale ambayo waheshimiwa wengine wamesema. Naunga mkono asilimia mia na naona tumejadili vya kutosha; sikushurutishi lakini naona hata ukiuliza swali si vibaya. Asante mheshimiwa Spika.

*(Applause)*

**Hon. Baya:** Thank you Mr. Speaker. Allow me to be the last person so that we can save time. We read and understood the Report. Patience pays. Number two, just a simple submission, I thank you, our able Chairperson hon. Kiraga through the Office of the Clerk for a good job.

Second, we are ready to pass the budget so without delay, let us all agree and pass it. Finally, I support the Motion. Thank you, Mr. Speaker.

*(Applause)*

**Hon. (Ms.) Sidi:** Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity and allow me to be the last person to give my submission because I can see the mood of the House everyone is in

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*



agreement with the budget, I want to applaud the Committee on Budget and Appropriations for a job well done. It was a strenuous activity but finally we have a Paper that we can both agree on.

Moving forward Mr. Speaker, I have issues that I want to highlight; aware that our budget is programme based, I still have an issue that I want the Committee to really put into consideration especially on the programmes.

Are the programmes that are implemented gender responsive on matters budgeting? If they are not and we all know that the population of Kilifi is mostly densely populated with women, youth and people living with disabilities, I will urge the Committee that in the next budget we are going to embark into; it should be more of gender responsive.

The other issue I wanted to highlight also is about the soundness of the budget process; it was a strenuous activity and it went to a point even the House felt like the Budget Committee is staying so much outside of this House. I want us to have a sound budget process; a process that is transparent, realistic and comprehensive in a manner that once we receive the budget we will not even have much time to spend outside. We should have a budget that is able to speak for itself. With those few issues, I support the Motion on the adoption by the Budget and Appropriations Committee. Thank you very much Mr. Speaker.

*(Question put and agreed to)*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): That does not mean the budget has passed; we are still on with the process. Next motion!

ADOPTION OF THE REPORT ON THE VETTING OF THE NOMINEE TO THE POSITION OF  
CHIEF OFFICER, ENVIRONMENT AND NATURAL RESOURCES

**Hon. Hassan:** Thank you Mr. Speaker Sir. I beg to move the following Motion:-

THAT, this House adopts the report of the Committee of Water, Environment and Natural Resources on the vetting of the nominee for appointment to the position of Chief Officer, Environment and Natural Resources laid on the Table of this House on 27<sup>th</sup> June, 2018.

Let me kindly call upon hon. Mwamtsi to second the Motion. Thank you, Mr. Speaker.

**Hon. Mwamtsi:** Mr. Speaker, I am among the Committee Members that sat and vetted madam Maryam for this position. Mr. Speaker, the curriculum vitae...

*(Hon. Mwamtsi spoke off record)*

Mr. Speaker, I think these electronic gadgets needs some maintenance; they are making the debate not to move smoothly.

Mr. Speaker, I was among the Committee Members that vetted madam Maryam for this position. When you go through the CV, the experience, the education and the interaction that she has, she is going to be a better person for this position. In Kilifi County, issues of environment are enormous from garbage collection, dust in Athi River which is killing many of our people, to the salt firms in Magarini and minerals in Jaribuni. We need this Chief Officer. We questioned Madam Mary Mariam and the answers and responses she gave convinced us and we can stand up here and support her in this position. So I do not want to talk much. I am urging my fellow hon. Members to support madam Mariam to this position. Thank you, Mr. Speaker.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

*(Question proposed)*

**Hon. Shaban:** Asante sana mheshimiwa Spika. Mimi pia nimesimama kuunga mkono Ripoti hii. Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja wa wanakamati ambao waliweza kumkagua huyu mama. Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza tutapata *Chief Officer* ambaye atakuwa na bidii na kufanya ile kazi ambayo atakuwa amepata.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na shida ya maswala ya takataka katika miji yetu na tulipomhoji mama huyu, alikuwa mjasiri na akasema shida hii ataweza kuitatua atakapopata nafasi hii. Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono Ripoti hii na naunga mkono kwamba huyu mama apewe kazi hii ili aweze kutatua tatizo hili la taka na matatizo mengine ambayo yanawakumba wakaazi wa Kilifi. Asante.

**Hon. Mwarandu:** Thank you so much Mr. Speaker. I think the Chairperson of the Committee on Water, Environment and Natural Recourses is crossing his fingers not to hear what he thinks I want to say but I think today is a very different case.

Mr. Speaker, I stand to support the Motion. I think Mr. Speaker; I am slowly coming to like the Governor because by nominating Mariam Jeneby, I think the Governor has shown an interest of empowering women of this County.

Number two; as a student of history, I want to inform this House that Mariam Jeneby is the daughter of Ahmed Mohammed Jeneby the first Member of Parliament of the larger Lamu-Tana River region and he was elected through Shungwaya Freedom Party that was affiliated to Kadu then and now Kadu Asili.

*(Laughter)*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Thank you for the history lessons.

**Hon. Mwarandu:** You are welcome. Mr. Speaker, still in history, Mr. Jeneby and Ronald Ngala and one Mr. Abdililahi Nassir Sambuli were the only people who represented the Coast ten mile strip in the Lancaster House. So by nominating Mariam Jeneby, the Governor has also shown he honours the heroes and heroins of this County. Thank you, Mr. Speaker.

**Hon. Mwayaa:** Asante mheshimiwa Spika. Mimi nami nilikuwa ni mmoja wa waliokuwa wakaguzi wa Mariam Jeneby. Kusema kweli, Jeneby alionyesha ujasiri katika mahojiano kwenye ule mkutano wa Kamati yetu. Mariam Jeneby ni msomi na amefanya kazi katika Idara mbali mbali na yeye mwenyewe alikuwa mwalimu na tulivyokuwa tunamhoji, tukamwambia kwamba kuna maswala tunayosema '*conflict of animals*' na binadabu; alilijibu vizuri hilo swali na akasema itabidi tuweke mipaka na chochoro za wanyama ili hili swala liweze kuzuiliwa.

Mheshimiwa Spika, Mariam Jeneby alionyesha ujasiri na makaratasi yake yanafaa kabisa akawe *Chief Officer* wa Idara ya Mazingira. Mheshimiwa Spika, naomba Bunge hili tumpitise na tutakuwa tumepata mtu mwenye ufahamu katika nyanja hiyo. Asante mheshimiwa Spika.

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Thank you hon. Members. The Motion has been moved and the same has been deliberated. I now put the question.

*(Question put and agreed to)*

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ADOPTION OF THE REPORT ON THE VETTING OF THE NOMINEE  
TO THE POSITION OF CHIEF OFFICER; PUBLIC SERVICE MANAGEMENT

**Hon. Kadenge:** Thank you Mr. Speaker. I beg to move a Motion:-

THAT, this House adopts the Report of the Committee on Administration, Labour and Social Services on the vetting of the nominee for appointment to the position of Chief Officer, Public Service Management laid on the Table of the House on 27<sup>th</sup> June, 2018. Before I call my able Vice Chairperson to second, I would like to make some few remarks which I will start with the criteria which we were using while vetting Vincent Mwalimu.

First we had to check his bio data; which we confirmed through his identity card that he is a resident of Kilifi County. Then we went again to his academic qualification which we confirmed through his originals that he holds a Masters of Human Resource Management from the Jomo Kenyatta University which is a big plus in the position he is applying. We also checked his employment record and we realized he is currently working in the Kilifi County Assembly as a Committee Clerk which by giving him this position will be a link between the County Assembly and the Executive which is a song we have been singing for a long time.

Again, we went ahead and checked his professional affiliation and we confirmed that he had several certificates which I will not mention because they are so many that I cannot read all of them but finally, we looked at his integrity and he produced a police clearing certificate and the clearance from Higher Education Loans Board (HELB) and the Ethics and Anti Corruption Commission (EACC).

Giving Vincent this position we will be also empowering the youth. So I beg this honourable House to pass this Motion and give a chance to Vincent Mwalimu to work in this great County of Kilifi. With those few remarks, I would also wish to thank the Office of the Clerk, especially my two able Clerks, Habel and Charity, for their support towards this journey of vetting Mwalimu. Thank you Mr. Speaker and I want to call upon the able Deputy Chairperson to second the Motion. Thank you.

*(Hon. Shaban seconded)*

*(Question proposed)*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Yes.

**Hon. Hassan:** Asante mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii...

*(Hon. Shaban stood to speak)*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): No! No! It is okay you will continue. No problem...

**Hon. Hassan:** Mimi binafsi nimesimama kuunga mkono Hoja hii iliyowekwa na Mwenyekiti wetu wa Leba kwamba huyu kijana ndugu Mwalimu anastahiki katika hiyo nafasi. Mheshimiwa Spika, utakubaliana na mimi kwamba huyu kijana amepeana changamoto kwa Bunge hili kwa sababu haikuwa ni rahisi kwa mtu ambaye alikuwa ni *Clerk Assistant* na sasa hivi kutaka nafasi kubwa kama hiyo na hapo ndipo nilipoamini kwamba kumbe mwili unaweza kuwa mdogo, lakini akili ikawa ni kubwa. Kwa hivyo, kwanza binafsi nampongeza huyu kijana kwa bidii na hii nafasi hakika tunastahiki tumchague.

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Mheshimiwa Spika, si yeye peke yake ambaye atakuwa ametoka hapa na kuweka historia ya Bunge hili la Kilifi. Kama tunavyofahamu kwamba tulikuwa na ndugu Mkare kama *Clerk* na tukampatia nafasi sasa hivi ni *County Secretary*. Tuliwahi kuwa na mheshimiwa sasa hivi ambaye ndiye *Woman Representative*; Mbeyu, alitoka Bunge hili na wengi tu. Kwa hivyo, ni changamoto kwa wale wengine waliobaki na wao wafanye bidii ili kutimiza malengo yao ya baadaye. Kwa hivyo, kwa unyenyekevu ningeomba waheshimiwa kwamba huyu kijana tusimnyime hii nafasi; tumpatie hii nafasi kwa mikono miwili ili aweze kutuhudumia kwa upande ule mwengine. Kwa hayo machache, mheshimiwa Spika, nimesimama kuunga mkono asilimia 100. Asante.

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Hon. Dickson (Shaban)

**Hon. Shaban:** Asante sana mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono Ripoti hii ili tuweze kumuidhinisha Vincent Lugwe kuwa *Chief Officer*. Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimshukuru mheshimiwa Gavana kwa kutuletea jina hili kwa sababu Vincent ni kijana ambaye amejikakamua kuhakikisha pale yuko leo. Mheshimiwa Spika, unakuta wakati mwengine nafasi hizi zinapewa watu ambao umri wao ni mkubwa lakini tunapata kijana ambaye anaenda ofisi ile na tuna matumaini kwamba akifika kule ataweza kusaidia watu wa Kilifi na hususan vijana. Mheshimiwa Spika, pia tunaona kuwa mheshimiwa Gavana amechagua huyu kijana kutoka *minority tribe*.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nimekuja Bunge kupitia *nomination ya minority*; ni kwamba nimetambulika. Na pia mheshimiwa Gavana ametuletea *Chief Officer* kutoka *minority tribe* ambayo ni *tribe* ya Jibana. Kwa hivyo, tunashukuru na sisi kama Bunge tungeomba kwamba tuweze kumuidhinisha kwa sababu kama ni elimu, kijana amesoma vizuri kama vile *Chairperson* ametwambia amesoma chuo cha *Jomo Kenyatta University* ambayo ni *University* ambayo inasifika sana. Kama ni *experience*, kijana amekuwa na *experience*; hata amefanya kazi hapa Bunge. Kwa hivyo, mimi naomba waheshimiwa tumpitishie ili aweze kuanza hiki kibarua na tumtakie kila la heri. Asante sana mheshimiwa Spika.

**Hon. (Ms.) Maneno:** Asante sana mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii. Mimi pia nimesimama kuunga mkono Ripoti hii ya kupitishwa kijana ambaye anaitwa Vincent Mwalimu Lugwe. Bwana Spika, ni kweli kama ambavyo mheshimiwa Shaban ameeleza, kwamba ni kijana ambaye anastahili kupata kazi hii ili turudishe imani kwa vijana wetu wa Kilifi Kaunti. Pia, tukiangalia ametoka kwa kabila dogo; kwa kimombo tunaita *minority*. Tukiangalia, Kilifi Kaunti tuko na *minority*; wa Kambe, wa Ribe na wa Jibana. Hivyo basi, tumerudisha hata pia moyo wa shukrani katika eneo la Jibana. Bwana Spika, nimesimama kuunga mkono Ripoti hii. Asante.

**Hon. Chengo:** Asante sana mheshimiwa Spika kwa kunipatia ...

*(Hon. Chengo spoke off record)*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Members, press the intervention button. If you press the other one, the system is malfunctioning.

**Hon. Chengo:** Asante sana mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi ili kunena machache kuhusu huyu kijana. Nilikuwa mmoja wa wale ambao waliweza kumchunguza ama kumhoji na tulipata kwamba kijana ni mzuri sana na anaelewa mambo haya ya kuajiri watu na hata pia kuwasimamia. Ndiposa tuliweza kumpitisha kwa sababu tuna imani na huyu kijana kwamba anaweza kufanya makuu na akafanya mabadiliko mengi katika hali yetu ya uajiri hapa Kaunti

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

yetu ya Kilifi. Kwa hivyo, nimesimama kuunga mkono kwamba tuweze kumpitisha huyu kijana na aweze kutufanyia kazi nzuri katika Kaunti yetu na nasema asante.

**Hon. Changawa:** Asante mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii. Sikutaka kuongea sana leo lakini kwa sababu ya uteuzi wa Lugwe Mwalimu ambaye kwa kimo naweza kuwa sawa na yeye na pia kwa umri. Nataka kushukuru sana kwa nafasi hii ambayo ofisi ya Gavana imeamua kumtunuku Lugwe Mwalimu. Nimesimama kuunga mkono na pia ni heshima kwa Bunge hili kupitia kwa kiongozi wao Spika Jimmy Kahindi ya kwamba saa hii huenda kule tunakoenda na nikiangalia *Executive* ya Kilifi Kaunti, itafikia mahali ya kwamba wafanyaji kazi wote watakuwa wanatoka hapa kuenda kule ili utendajikazi wa Bunge na *Executive* uwe vizuri zaidi.

Hata hivyo, niko na masikitiko kidogo kwa sababu Lugwe ananiacha na Lugwe ni...

*(Hon. Changawa spoke off record)*

Lugwe ni *Clerk* wangu katika ile Kamati ya Elimu. Nimekuwa na yeye kwa muda ule wote. Ni kijana ambaye hana dharau; ni kijana ambaye kwa kufanya kazi ni namba moja. Kwa hivyo, nasema ya kwamba aende kwa hiyo *promotion* ili mwengine kama yeye apatikane na utendaji kazi uwe vizuri pia. Asante sana mheshimiwa Spika.

*(Question put and agreed to)*

## BILL

### *First Reading*

THE KILIFI COUNTY APPROPRIATION BILL, 2018

*(Order for the First Reading read – Read the First Time - Ordered to be read the Second Time today by leave of the House)*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Next order!

### *Second Reading*

THE KILIFI COUNTY APPROPRIATION BILL, 2018

*(By leave of the House)*

**Hon. Kiraga:** Thank you so much Mr. Speaker. Pursuant to provisions of Standing Order No. 121, I beg to move the following Motion:-

THAT, the Kilifi County Appropriation Bill 2018, be now read a Second Time.

Mr. Speaker, the Kilifi County Appropriation Bill, 2018, was read a First Time on Wednesday, 27<sup>th</sup> June, 2018. The Kilifi County Appropriation Bill, 2018 makes provisions for giving statutory sanctions for public expenditure for the year ending 30<sup>th</sup> June, 2019 on the basis

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

of the estimates for expenditure 2018/2019 development and for the appropriation of these amounts.

Mr. Speaker, even before I give it to the seconder, it is very important for this Bill to go for the Second Reading bearing in mind that the County Executive cannot spend even a single cent before the passage of this Appropriation Bill.

Therefore, by going to the Second Reading, it will now pave way for the Third Reading Mr. Speaker. I therefore call upon hon. Chiriba to second. Thank you.

*(Hon. Chiriba seconded)*

*(Question proposed)*

**Hon. Chiriba:** Thank you Mr. Speaker for this opportunity. I stand to support the passage of this Appropriation Bill and as the Chairperson has briefed this House that the passage of this Bill is very crucial, simply because it is the same that will authorize the monies to be spent as seen or spread on the several voteheads that I think hon. Members have copies of the same.

Mr. Speaker, I ask the hon. Members to consider this to be very urgent so that we may quickly pass the same since there are various Departments which are waiting for this to give them authority to use various sums of monies allocated to them. This focuses on the recurrent expenditure and also the development part and I pray that we will be in agreement as far as these monies is allocated in areas like Education Sector which focuses on both administrative and the capital funds authorized by this document. I pray that this honourable House will join hands so that we may quickly pass this document. Thank you, Mr. Speaker. I beg to support.

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Thank you hon. Members. The Motion has been read and deliberated. I now put the question.

*(Question put and agreed to)*

## COMMITTEE OF THE WHOLE HOUSE

*(Order for Committee read)*

*[The Speaker (Hon. Kahindi) left the Chair]*

## IN THE COMMITTEE

*[The Chairperson (Hon. Kenga) took the Chair]*

## THE KILIFI COUNTY APPROPRIATION BILL, 2018

**The Chairperson** (Hon. Kenga): Good afternoon hon. Members. Welcome to the Committee of the Whole House. We are now considering the Kilifi County Appropriation Bill, 2018. In this regard, you will realize the rules are a bit relaxed. You are in a position to consult

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

although we encourage constructive consultations that are within the provisions of the Standing Orders of the County Assembly. Clerk, please take us through the Clauses.

*(Clause 3 and 4 agreed to)*

*(The First Schedule agreed to)*

*(The Second Schedule agreed to)*

*(Clause 2 agreed to)*

*(The Short Title agreed to)*

*(The Long Title agreed to)*

Thank you very much Hon. Members. We have now successfully come to the end of the deliberations in the Committee. I call upon the Mover to proceed.

**Hon. Kiraga:** Thank you Chair. I beg to move that the Committee do report to the House its consideration of the Kilifi County Appropriation Bill, 2018, and its approval thereof without amendments. Thank you.

*(Question Proposed)*

*(Question put and agreed to)*

*(The House resumed)*

*[The Speaker (Hon. Kahindi) in the Chair]*

## **REPORT AND THIRD READING**

### THE KILIFI COUNTY APPROPRIATION BILL, 2018

**The Chairperson** (Hon. Kenga): Thank you very much hon. Speaker. I beg to report that the Committee of the Whole House has considered the Kilifi County Appropriation Bill, 2018 and approved the same without amendments. Thank you.

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Yes, hon. Kiraga.

**Hon. Kiraga:** Thank you so much hon. Speaker. I beg to move that the House do agree with the Committee in the said Report. I call upon hon. Chai Chiriba to second.

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Yes, hon. Chiriba.

**Hon. Chiriba:** Thank you Mr. Speaker for giving me this opportunity. Mr. Speaker, I stand to support the passage of this Appropriation Bill. Hon. Members, in this Bill we will give the authorization of the uses of funds to the different vote heads and the allocations since no

**Disclaimer:** *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

implementation can be done without the passage of the same and I call upon hon. Members that we may join hands and pass this Appropriation Bill. Thank you.

*(Question proposed)*

*(Question put and agreed to)*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Yes, hon. Kiraga.

**Hon. Kiraga:** Hon. Speaker, I beg to move that the Kilifi County Appropriation Bill, 2018, be now read a Third Time. I call upon hon. Pascal to second.

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Yes, hon. Pascal.

**Hon. Pascal:** Thank you Mr. Speaker for giving me an opportunity to also ventilate on the same. Mr. Speaker, I also support that the Bill to be read a Third Time because this is what will culminate into the passage of this Bill. It is only the last process of the Bill that we need to actually confirm as a House so that we give an opportunity to the various Departments to spend these monies. Therefore, I call upon hon. Members to actually agree and support the Motion on the Floor.

*(Question proposed)*

*(Question put and agreed to)*

*(The Bill was accordingly read the Third Time  
with leave of the House and passed)*

**The Speaker** (Hon. Kahindi): Hon. Members, having been read for the Third Time, now the Bill is ready for submission to His Excellency, the Governor, for assent.

### ADJOURNMENT

In the absence of any other Business in the Order Paper, I move to adjourn the House until next week. Thank you very much.

**The House rose at 4:46 p.m.**